

Ljumaa Januari 20, 2023

# Waziri Mkenda ashtukia jambo digrii udokta wahitimu wa nje

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameipa rungu Bodii ya Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) kuchunguza ubora wa elimu na kutuma timu ya wataalamu kuhakiki tuzo zinazotolewa na baadhi ya vyuo vya nje.

Waziri Mkenda alitoa agizo hilo jana mjini hapa wakati akizindua bodi hiyo.

Alisema lengo ni kuwapa taarifa zilizosahihi Watanzania wanaotaka kupeleka watoto wao kusoma vyuo hivyo kwa kuwa ni jukumu la TCU kuwezesha na kudhibiti ili ubora wa elimu usiteterere. "Lengo si kuzua wanafunzi kwenda kusoma kwenye vyuo hivyo bali kutoa taarifa kwa Watanzania kuhusu ubora wa tuzo zinazotolewa na vyuo hivyo hasa vinayofundisha masuala ya udaktari, nilishaongea na balozi mbalimbali si vizuri kuzitaja timu iende na Katibu Mkuu kuangalia baadhi ya vyuo vi-kuu duniani ili kuhakiki," alisema.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya vyuo vinafundisha udaktari kwa njia ya mtandao na kueleza kuwa hajui kama vinamwandaa vizuri daktari kuja kufanya kazi nchini.

Aliagiza wahadhirii wanaoajiriwa ambao wana elimu ya Shahada ya Umahiri (Masters), kuwasilisha maandiko yao watu wasikilize.

"Kuna sehemu kubwa inatutaka kufanya ili kuongeza ubora, sehemu moja wapo vyuo vi-kuu vinafundisha walimu ambao wanakwendwa kufundisha huku chini, halafu huku wanasema watu wanaohitimu vyuo vikuu hali si nzuri, kwa hiyo ni mzunguko kwa hiyo, vyuo vikuu ni muhimu kusimamia ubora wake kwa kuwa itakuwa ni chachu ya kusaidia kuongeza ubora huku chini," alisema.

"Kwa mfano tunapoajiri wahadhirii vyuo vi-kuu tusiangulari tu GPA tunaziamini, lakini kuna mambo mengi kuhusu GPA, tuwe na mahojoano, lakini na uwasilishaji lipo kwenye kanuni za TCU tusimamie.

"Kuna mtu alikuja kipindi kile nipo chuo kikuu akaja kuwasilisha andiko lake, lakini wakati tunampiga maswali tukajua huyu bogus (hana kitu), akaishia kusema ameandika haraka wakati sio kweli, alivyoodoka tukaangalia cheti amesema Norway na hana PhD kama alivyokuwa akisema."

Aliwakumbusha kuangalia suala la udanganyifu kwenye maandiko ya ngazi za elimu kuu wanaohitimu kutokana na baadhi yao kuanzisha ofisi za kuwaandikia watu.

"Napendekeza kwenu mfanya utaratibu wa kuchukua utafiti wao siku hizi kuna mfumo wa kutambua kama utafiti huo ni wa mtu, na ukipata hilo unatangaza kwa umma na aibu kwa chuo husika na msimamizi wa utafiti, unakuta muntu anasimamia watu 20 unawezejie?" Alihoji.

"Hizi ni salamu za vyuo vikuu tunataka hizi tuzo zihakiki, kwenye shahada ya Uzamivu ni vyema kuwe na utaratibu wa kutoa mawasilisho yao hadharani na umma usikilize badala ya watu wachache kujifungia kumpitisha kuperwa tuzo ya PhD," alisema.

Mwenyekiti wa Bodii ya Tume hiyo, Prof. Penina Mlama, alimhakikishia Waziri Mkenda kuwa watatekeleza maelekezo yote aliyowaaigiza na kujifungua nchi kimataifa kwa kuwapeleka wanafunzi wengi kusoma vyuo vya nje ya nchi.

Prof. Mlama alisema bodi hiyo itahakikisha vyuo nchini vinasimama vyema kitaaluma kuhimili na kuyamudu mabadiliko ya kasi yanayotokea katika sekta zote za maendeleo binadamu, siasa, kiuchumi, kijamii na sayansi.